https://dspace.org/

# Utendi Wa Ramani Ya Maisha Ya Nrowa (Mume) Uliyotungwa Ni Usadh Mahmou Ir (Mau) Wa Lamu, Kenya

**Karama, Mohame**

**2023**
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/595

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

**UTEṆḌI WA RAMANI YA MAISHA YA NROWA (MUME)**
**ULIYOTUNGWA NI**
**USṬADH MAHMOUḌ A. ABDULQAḌIR (MAU) WA LAMU, KENYA**

1. K̇a ina la Rahamani
Naaṇḍa nudhuma hini
Ina ya pili ramani
Naṁaṇḍikiya Yahaya.

2. K̇enye ramani ya k̇aṇḍa
Banaṭi naliwafuṇḍa
Na hini nimeiyunra
Wavulana kuwambiya.

3. Na asili ya k̇aṇḍika
Nahisi wana waṭaka
Baba piya kadhalika
Mimi alinaṇḍikiya.

4. Baba Ḃana Ahmaḍi
Aṭamjazi Waḍuḍi
K̇ani alijiṭahiḍi
Kunaṇḍikiya wasiya.

5. Hapo Zamani za Yana
Nriyo la wasiya yina
Alonaṇḍikiyya ḃana
Babangu kaniwaṭiya.

6. Nami katika ramani
Ṭʰayipiṇḍa kubaini
Yale ninayoamini
Yaweza kusaiḍiya.

7. Ṭʰanena naloyaṭuma
Na yale niloyasoma
Ṭʰazitaya na hekima
K̇a watʰu nilopokeya.

8. Yale niṭayokusanya
Mbali mbali kuṭanganya
Lengo langu ni kufanya
Kama la maisha boya.

9. Boya hili la maisha
Kaṭu haliṭozamisha
Ashikao ṭamvusha
Baṇḍari ṭasikiliya.

10. Ṁanangu ukiyazimu
Kuwowa k̇aṇḍa fahamu
Kuṭauwa ni muhimu
Ni amri ya shariya.

11. Mtumi alibaini
Akaṫambiya owani
Ṁanamke ṁenye ḍini
Mungu ṭawabarikiya.

12. Ṁanangu siṭake mke
K̇a wema wa umbo lake
Nasaba na pato lake
Mayuṭoni uṭangiya.

13. Wala ḍini haineni
Owa shuguu la uni
Kishuna kilo na ḍini
Kukiyowa si haṭiya.

14. Ṁenye nasaba ṭukufu
Na k̇a Mola mṭiifu
Hawi mtʰu mekhalifu
Kama huyo kuzengeya.

15. Na mke alo na chake
Sik̇ambii simṭake
Bora awe ḍini yake
Meshika hakumbiriya.

16. Ḍini ni kama bureki
Humziwiya haṭoki
Mipakani na haruki
Akiwa ṭaitumiya.

17. Na ḍini humziwiza
Kutenra yasopeṇḍeza
Na nripo kakuhimiza
Ṁenye ḍini k̇angaliya.

18. Ḍini ninayoinena
Sikuwa nayo ni ina
Ḍini ni k̇aṇḍama sana
Amri zake Jaliya.

19. Ni ḍini k̇enye maisha
Mtʰu iwe huṁenresha
Si ḍini ya kwonesha
Watʰu kuwahaḍaliya.

20. Ni ḍini iliyo nrani
Iliyokita moyoni
Nriyo huwa ni sukani
Ya kumwongoza ṇḍiya.

21. Na ukisa k̇amuwa
Ni fulani ṭamuwowa
Fanya mambo sawasawa
Saṇḍame ya jongo ṇḍiya.

22. Usifanye ya sheshegi
Kama watʰu wenye gogi
Siipeke zigizagi
Harusi nimek̇ambiya.

23. Kula ikiwa ni pesi
Huwa ni bora harusi
Fanya mambo ya kiyasi
K̇a gharama ngoma piya.

24. Makubwa usiyaṭake
Na mipaka usiruke
Piya upanre wa mke
Waeleze kama haya.

25. Zikiwa nyingi gharama
Na mayuṭo ni lazima
Ngoma zikisa kukoma
Ni lawama husaliya.

26. Fanya mambo ya kaḍiri
Siṭake mno fakhari
Nakuusiya sikiri
Hafula za maasiya.

27. Hafula za isirafu
Na za magoma machafu
Na kuwa tutu k̇a ufu
Ḍini hayo huzuwiya.

28. Mila yetu usiwaṭe
Mfano kuvisha pete
Si yetu usifuwate
Wengi wangakazaniya.

29. Ni mila ya kinasara
K̇iwaṭa nriyo bora
Wangawa waṭakukera
Waja k̇a kuṭoeleya.

30. Na k̇enra kupa mkono
Usikiri ṭangamano
Haṭa alo nruyo mno
Simuwaṭe nawe kuya.

31. Nyumba yako siyasisi
K̇a msingi wa maasi
Ṭaivutiya nuhusi
Na ukorofi kungiya.

32. Na maasi ninenayo
Ni kula mambo ambayo
Mola ayaṭukiyayo
Na kula aloziwiya.

33. Moya moya siṭoweza
Kutonrowa kuk̇eleza
Nimekupa ṁangaza
Wa ṇḍiya kufuatiya.

34. Nimekupa ni kiyasi
Kitumyie nawe basi
K̇a mangineyo kukisi
K̇a mizani kutumiya.

35. Nyumba njema ni msinji
Ṭamu ya chai si ranji
Wengi metiliwa ṭanji
K̇a fakhari kuzengeya.

36. Kiwa ni lazima sana
Hilo la k̇aṇḍamana
Shemegiyo mvulana
Aṇḍamanani pamoya.

37. Au ṁengine yoyoṭʰe
Maharimu nafuate
Ajinabu simuwaṭe
Mkeyo kuṁangaliya.

38. Rafiki siṁamini
Ukamtiya nyumbani
Ila dharura fulani
Sikuye ikiṭokeya.

39. Rafiki usimliche
Ni zaiḍi huyo mche
K̇a wao mambo ya cheche
Huwa usolidhaniya.

40. Zizini kutiya simba
Ni kama moto na pamba
Mara moya huzisumba
Na yivu likasaliya.

41. Rafiki kingiya nrani
Sikuye ukaṭamani
Sambe ona ni nyumbani
Hee! Utayiṭongeya.

42. Hiyo k̇etu siyo mila
Kungiya kula mahala
Pasi hoḍi na sumila
Siyo yetu mazoweya.

43. Yali na kazi maḍaka
Ni wageni kuwaḍaka
Maḍaka ni kuwaweka
Na nrani kuṭoṭungiya.

44. Ila awe ni mgeni
Wa kushukiya nyumbani
Hungiya na hamuwoni
Aliyo nrani mmoya.

45. Na uchenra safarini
Kashukiye hotelini
Sipeṇḍe sana nyumbani
Ila ni kupita ṇḍiya.

46. Ukiṁenreya nyumbani
Ṁenye tʰotʰo masikani
Au alo masikini
Ṭaabuni humtiya.

47. Na iwapo huna buḍi
Hukufanya k̇a kasiḍi
Siku tatu usiziḍi
Siyongeze haṭa moya.

48. Na hilo wewe sitenre
Ila mambo yakushinre
Mṭeremko sipeṇḍe
Nyongo hukutumbukiya.

49. Lojingi kiwa hapana
Au mfukoni huna
Nenra k̇a hadhari sana
Kama kupoṭeya ṇḍiya.

50. Kiwa mtʰu mek̇alika
Ni wajibu k̇itika
Shughuli kimalizika
Musiweke mazoweya.

51. Na wewe k̇ako nyumbani
Siifanye mno ḍuni
Kuwa mtʰu wasiṭani
K̇a mapambo kuyitiya.

52. Mtiliye mke wako
Zitʰu k̇a kaḍiri yako
Ikiwa nafasi iko
Sibane ukaziwiya.

53. Iwe mariḍaḍi nyumba
Na k̇a zitʰu k̇ipamba
Fesheni ambazo k̇amba
Kama yeye hutumiya.

54. Mtiliye kula kitʰu
Awe kama weṇḍe watʰu
Siṁambiye mimi k̇etu
Haya sikuyazoweya.

55. Akiwa mbwa minazini
Ukimuweta muyini
Simuwaṭe kuṭamani
Za weṇḍe kishuhuḍiya.

56. Ukiwa umeamuwa
Muyini kumṭukuwa
Mfanyiye sawasawa
Sambe si ya k̇enu haya.

57. Siṁambiye zitʰu hizi
K̇enu kupata huwezi
K̇enu ni kama kizizi
Hukuwona mazuliya.

58. Na chakula kadhalika
Mpe anachokiṭaka
Ambacho ṭafurahika
Ṁenyewe mekizoweya.

59. Akipeṇḍa biriyani
Mpe ṁana simkhini
Maaḍamu mfukoni
Akiba imesaliya.

60. Siku akiṭaka sima
Siṁambiye ewe mama!
Kula mṭee lazima
Mimi siṭaki udhiya.

61. Ṁaṭiye na khiyari
Apeṇḍacho akhiṭari
Simkaze si uzuri
Masharuṭi kuṁekeya.

62. Ila kilicho haramu
Hilo sikiri fahamu
Haramu na kula sumu
Shariya imeziwiya.

63. Ama kuhusu mavazi
Ya kaye na siku hizi
Sikiri ya k̇enra wazi
Mishono yaso na haya.

64. K̇etu sisi Isilamu
Mavazi kitʰu muhimu
Na sisi yatulazimu
Ya zipimo k̇angaliya.

65. Mpe ṁenyewe nafasi
Ya kuṭauwa libasi
Lako wewe ni fulusi
Ṭowa za kununuliya.

66. Mpe yako masharuṭi
Za mshono kudhibiṭi
Akikhalifu mehiṭi
Ni haki kumziwiya.

67. Ama kiṭambaa gani
Kikuuliza ṁeṇḍani
Au ni ipi launi
Wewe waifurahiya.

68. Hapo makosa hapana
Kikuuliza kunena
Rangi hini naiyona
Maṭoni imeningiya.

69. Ama kiwa ni ṭamasha
Waṭaka mfurahisha
Si haja kumwonesha
Maoniye k̇angaliya.

70. Kata uṭakachopeṇḍa
Umṭunukiye nyoṇḍa
Nawe hili ukitenra
Chochoṭʰe ṭakongoweya.

71. Mke wako simdhiki
Siṁambiye sina hiki
Na nyingi mno siṭaki
Sizoweye kutumiya.

72. Mpe k̇a yako kaḍiri
Usifanye ṭaqiṭiri
Ni ṭwabiya si mzuri
Ubakhili k̇enye haya.

73. Na wewe upanre wako
Ipambe kiyasi chako
Bora usivuṇḍe miko
Khaṭiyani ukangiya.

74. Kuwa mtʰu mariḍaḍi
Uṭunge yako jasaḍi
Haṭa kufukiza uḍi
Ukiweza si khaṭiya.

75. Iweke uwe nadhifu
Siyonekane mchafu
Hini ni sunna ṭukufu
Ya Tuṁa wetu nabiya.

76. Kiwa nyee umeweka
Zangaliye kadhalika
Siwaṭe kusokoṭeka
Shungururu kusaliya.

77. Ikiwa wafurahika
Mkeyo akipambika
Yuwa na yeye huṭaka
Nawe uwe huvutiya.

78. Hiyo naye ṇḍake haki
Ṭakuwa hafurahiki
Iwapo hushughuliki
Ṁilio k̇angaliya.

79. Naye piya huṭamani
Akikuwona ṇḍiyani
Uwe nawe hisabuni
Penye watʰu uṭangiya.

80. Au kiwa yako kazi
Kutenra haya huwezi
Wisapo vuwa magozi
Sivaye kuṭembeleya.

81. Siṭembee na magwanra
Wala harufu za ng’onra
Fahamu watʰu huṭuṇḍa
Na akilini hutiya.

82. Na kadhalika ulimi
Ipinre uwe husemi
Yalo mawi huwaṭami
Mke wako kuṁambiya.

83. Mno sana jiṭahiḍi
K̇a maneno mariḍaḍi
Wake huṭaka zaiḍi
Yalo ṭamu kusikiya.

84. Nena naye k̇a dhihaka
Afurahi akicheka
Ṁanamke huudhika
Mno kumnyamaliya.

85. Mfanyiye na ubishi
K̇a maneno yaso ghashi
Na k̇ake kuwa mṭeshi
Bila ya kupinrukiya.

86. Ṁanamke ahiṭaji
Kuvishwa la sifa ṭaji
K̇a hilo kuwa mpaji
Usichoke kuṁambiya.

87. Ṁambiye kula namna
Sifa zake ṭena sana
Mfano ukimuwona
Nyee mefunga upiya.

88. Kiwa mesuka mikili
Au kuruni mawili
Siliwaṭe yambo hili
Bila ya kulitumiya.

89. Ṁambiye umepeṇḍeza
K̇a nyee kuzitengeza
Sina buḍi ṭakutuza
Umshumu mara moya.

90. Kiwa ametiya waṇḍa
Ṁambiye mno napeṇḍa
Siifanye hukuṭuṇḍa
Au hukuṁangaliya.

91. Kijifunga asumini
Au kikuba kiṭwani
Sichelewe kubaini
Neno lema kuṁambiya.

92. Yaani kula wakaṭi
Ṁambiye kitʰu kaṭiṭi
Na kama bubwi sikeṭi
Au ḍuko ṭʰongo piya.

93. Piya mpe shukurani
K̇a shughuli za nyumbani
Mfano pilau hini
Mno umeipatiya.

94. Usichʰoke kumsifu
K̇a nyumba kuwa nadhifu
Na ukiyona uchafu
Usiwe ṭamuukiya.

95. Na faragha ukipata
Mbee yako kikupita
Usiwe uṭamuwaṭa
Mkono kumpekeya.

96. Mshike wake mkono
Wala simkaze mno
Huṭosha nukuṭa ṭʰano
Ujumbe kumpekeya.

97. Kiwa amekukabili
Siitiye mashughuli
Inuwa yako mawili
Na yake kuṁelekeya.

98. Waṭa maṭo yafumane
Kaṭiṭi yangaliyane
K̇a ulimi usinene
Lugha ya maṭo tumiya.

99. Maṭo yana lugha ṭamu
Hunena mukafahamu
Maṭo kiyungo muhimu
Cha huba kupaliliya.

100.Maṭo yana kʰuu siri
Na mara huk̇adhiri
Kakuṭoleya khabari
Moyoni uloziwiya.

101.Hili nimenena sana
Ni muhimu naliyona
Wala gharama halina
Na si kazi kutumiya.

102. Walakini si sahali
K̇a kila alo mvuli
K̇a wangine ni thakili
Kaṭu hawakuzoweya.

103. Mbinu hizi izoweze
Zitumiye sizipuze
Uṭaona faiḍaze
Ṁenyewe ṭashuhuḍiya.

104. Mambo hayana gharama
K̇angaliya na kusema
Na mtʰu mke ḍaima
Kama haya huzengeya.

105. Mke huwa una ṁako
Kuyuwa maoni yako
Kusikiya neno lako
Ni haja ahiṭajiya.

106. Yuwa haṭosheki mke
Kuvaa na kula k̇ake
Ataka na utʰu wake
Na hishima kuṁekeya.

107. Kula alo mtʰu mke
Hili nrilo umbo lake
La mapambo hilo k̇ake
Ni yambo meyazoweya.

108. Huṭokeya k̇a naḍira
K̇a hili wasoyikera
Hina hapeṇḍi kuchora
Na wala waṇḍa kutiya.

109. Hana hayo mashughuli
Ni kama mtʰu mvuli
Ya urembo hayajali
Wala hakuyazoweya.

110. Kiwa nawe wako mke
Hilo si shughuli yake
Basi nawe sisumbuke
Mashughuli kuyitiya.

111. Na lengine la dharura
Ifuṇḍe mno subira
Kuna mambo ya kukera
Maishani yaṭokeya.

112. Hakuna maisha ṭamu
Yenye raha ya kuḍumu
Mambo ṭakuwa magumu
Kiwa huṭovumiliya.

113. Kuna ṭamu na uṭungu
K̇enye huu uliṁengu
Yaliyaṇḍa haya ṭangu
Yalipoumbwa ḍuniya.

114. Hini nriyo kawaiḍa
Kuna raha kuna shiḍa
Nriyo ya maisha aḍa
Na watʰu huwapitiya.

115. Basi na k̇ako nyumbani
Siyote kuwa peponi
Maaḍamu hapo nrani
Si wewe pweke mmoya.

116. Mke wako si kivuli
Bali ni mtʰu wa pili
Una na yake akili
Una na alozoweya.

117. Usiṭake k̇a lazima
Kula yambo ukisema
Alikubali ḍaima
Papo hapo kuridhiya.

118. Ṁatiye makawaṇḍa
Anene anolipeṇḍa
Na k̇a huja kikushinra
Siwe vito ṭatumiya.

119. Ukiyona sawa ṇḍake
Ikubali uridhike
Na wala sikasirike
Mḍomo kumfungiya.

120. Kubali mezolinena
Umuunge ṭena sana
Na faiḍa uṭaona
Mambo ṭaaṇḍama ṇḍiya.

121. Na yeye kikasirika
Wewe usipanre shuka
Na akiziḍi onroka
Kishinrwa kuvumiliya.

122. Ṁanangu moto tizama
Hauzinyiki ḍaima
Bali huziḍi roroma
Kʰuni ukiutiliya.

123. Moto kiṭotiwa kʰuni
Uṭazinyika ṁeṇḍani
Na utesi wa nyumbani
Kʰunize ni neno baya.

124. Ziwiya wako ulimi
Siwe na ṁingi usemi
Ukinena hayakomi
Maneno hwenreleya.

125. Ziḍi na kuyikukusa
Ulimi kuṭoṭapasa
Zita zenu ziṭak̇isa
Moto mayi uṭatiya.

126. Na alo mume hoḍari
Kishinrwa yeye hukiri
Ili k̇epuka ḍothari
Ya ufa sini kutiya.

127. Sini ikingiya ufa
Hupunguwa zake sifa
Na mahaba nayo hufa
Ukiwa ṁingi udhiya.

128. Hakuna kaṭu hakuna
Kiyumbe kamili sana
Na watʰu huṭukuwana
Nripo waishi pamoya.

129. Kiwa lazima waṭaka
Mke alokamilika
Juwa na wewe hakika
Ṭakubiḍi kutimiya.

130. Aso tʰaa ni ṭʰomomo
Hunu ni k̇eli msemo
Watʰu hupitana zimo
Huziḍiyana ṭwabiya.

131. Mke kikukasirisha
Jaribu kuyikumbusha
Piya hukufurahisha
Mezani hini tumiya.

132. Usiyaone ya jongo
K̇a mema ukawa ṭʰongo
Sangaliye penye pengo
Kawaṭa paloṭimiya.

133. Huna buḍi kupuuza
Na mangine kuyamiza
Nripo muweze kufuza
Na maisha k̇enreleya.

134. Mke kitenra makosa
Kuṁambiya yakupasa
K̇a hishima na siyasa
Na hikima kutumiya.

135. Kosa kulisahihisha
Penye watʰu hujeresha
Ipinre kupurukusha
Faragha kizengeya.

136. Siṁambiye penye watʰu
Haukiri wake utʰu
Wala hutengezi kitʰu
Bali ni kinyume huya.

137. Kumsifu ni uzuri
Penye watʰu na dhahiri
Kulaumu ni k̇a siri
Nripo aṭakusikiya.

138. Ṁanaaḍamu kukosa
Ni yambo limetupasa
Ni sawa kuyikukusa
Mangine kuvumiliya.

139. Lisamehe kosa ḍogo
Kosa likiwa mzigo
Halipeleki kishogo
Zengeya nyengine ṇḍiya.

140. Ṭafauti za nyumbani
Ziwe ni siri za nrani
Siziṭowe hadhirani
Watʰu wakazisikiya.

141. Siri za nrani zibane
Usiṁambiye mngine
Wewe na yeye munene
Suluhisho kuzengeya.

142. Ila mukikosa buḍi
Kunena ikawabiḍi
Wazee wawasaiḍi
Hapo haiwi haṭiya.

143. Ṭafauṭi ikizuka
Ni mikono kuyaṇḍika
Yuwa ṇḍe ikiṭoka
Huzuwa nyingi balaya.

144. Khususwa siri za siri
Kunena ni k̇adhiri
Ila iwe ḍakiṭari
Suwali mewataiya.

145. Mambo ya ṭʰini k̇a ṭʰini
Yawe ni nrani k̇a nrani
Hayo muwe hamuneni
Ila yakiwaemeya.

146. Kiwa mno mewaganya
Mukashinrwa la kufanya
K̇a hapo siṭowakanya
Ushauri kuzengeya.

147. Ni bora uwe hoḍari
Na kushinrwa usikiri
Wala usiṭahayari
K̇a halali kutumiya.

148. Ni hiko hiko kitenro
Kiwa wa halali ṁeṇḍo
Haramu iweke kanro
Kaṭu kuṭokaribiya.

149. Wa haramu simguse
Kimuwona igegese
Haṭa nyangwani mpise
Saṇḍamane naye ṇḍiya.

150. Usenre haṭa karibu
Epuka hizo iqabu
Uṭapata na thawabu
Mkeyo kumngiliya.

151. Elewa sana elewa
Ni jukumu umepowa
Mkeyo kuṁisa ngowa
K̇a haya nimezotaya.

152. Mkeyo mṭosheleze
Haja yake amalize
Na shauku asisaze
Mparo ukaṁaṭiya.

153. Ongeza wako uyuzi
Wa kufanya hiyo kazi
Ṁeṇḍo kiwa hamalizi
Fahamu wamkoseya.

154. Huwa ni kʰuu dhuluma
Wewe ukisakukoma
Huṭaki geuka nyuma
Na yeye kumngojeya.

155. Simalize yako haja
Mngoje ṁise pamoja
Hili haṭaki mmoja
Ni nyoṭʰe hulizengeya.

156. Angaliya ufikiri
Kiwa ṁeṇḍo ṭaghairi
Na wewe penye baṇḍari
Baḍo nanga hujatiya.

157. Uṭakuwa hali gani
Usingizi huuwoni
Hali hiyo ubaini
Na ṁeṇḍo huṁiliya.

158. Aṭakuwa na mṭaro
Na dhiki mno na kero
Na hasira na mfuro
Kiwa huṭomridhiya.

159. Nyumba nyingi huvuṇḍika
Zikikosa muwafaka
K̇a ngono kuṭoṭosheka
Mke na mume pamoya.

160. K̇a hili mukiṭoshana
Mengi huvumiliyana
Mno hukorofishana
Hili lisipoṭimiya.

161. Na lingine kadhalika
Ambalo k̇ako naṭaka
Ni mkeyo kiyudhika
Usiwe ṭamfuriya.

162. Pangine uṭamuwona
Hufura sababu hana
Ṁelewe ṭena sana
Na mno kumuyuliya.

163. Ifahamu ṭafauṭi
Waliyo nayo banaṭi
Hawezi kuyidhibiṭi
Hali inapowaḍiya.

164. Mke si kiyumbe ḍufu
Walakini ni dhaifu
Moyo wake ni khafifu
Hushinrwa kuvumiliya.

165. Wanawake wana umbo
Hwathirika k̇a mambo
Kaṭiṭi yakenra kʰombo
Wasi wasi humtiya.

166. Katika siku za aḍa
Ya ṁezi hupata shiḍa
Nripo haṭa na ibaḍa
Mungu kawapunguziya.

167. Mno huwa ya thaqili
Na hubaḍilika hali
Na choṭʰe kiwiliwili
Huwa katika udhiya.

168. Huwa sana ni wayavu
Hukosa uvumilivu
Huwa kama ivu ivu
Kuṭumbuka huzengeya.

169. Huwa mno ni wakali
Nadhani haṭa akili
Haiwi sawa kamili
Na punguwani hungiya.

170. Kula mara ṭamuwona
Huwarukiya zijana
Na k̇a ukali hunena
Kinyume cha mazoweya.

171. Ni muhimu kula mume
Mke wake amsome
K̇a zipimo ampime
Siku zikikaribiya.

172. Ukisa kumfahamu
Uwaṭe kumlaumu
Hili mno ni muhimu
Yaṭaka kulizoweya.

173. Kuna na muḍa wa mimba
Mara k̇a mara huvimba
Ukaona kana k̇amba
Mekuwa hukuzengeya.

174. Kukosa yambo kaṭiṭi
Huwa wewe umehiṭi
Angaliya kibiriṭi
Kiḍarika ṭʰeṭe huya.

175. Mara nyama haiṭaki
Aṭaka nsi wa siki
Alacho hakimshiki
Akitiyacho huṁaya.

176. Ziyelewe siku hizi
Mimba na siku za ṁezi
Kiwa humbembelezi
Ṭaona wamuwoneya.

177. Mpembe kama kijana
Ṭena aliyo mnuna
Nripo muṭasikizana
Na yaḍumu mazoweya.

178. Sharuṭi uwe ṁerevu
Na mno mvumilivu
Usifurishe mashavu
Kiwa naye meteteya.

179. Kuna mambo ya umitʰo
Ni makuu si matʰotʰo
Wengine hula tʰotʰotʰo
Na mṭanga hubugiya.

180. Ni mambo ya miyujiza
Zao hali hugeuza
Kiwa huṭobembeleza
Mara ṭaona huliya.

181. Ṁanamke k̇a ṭaabu
Mara hufanya ghadhabu
Haṭa alo ṭaraṭibu
Hubaḍilika ṭwabiya.

182. Neno loloṭʰe aweza
Hajali kuvurimiza
Ni sharuṭi kuyikaza
Mizani kuṭopoṭeya.

183. Mara aweza ṭalaka
Akak̇ambiya naṭaka
Nawe ukikasirika
Mayuṭo yaṭasaliya.

184. Akik̇ambiya niwaṭa
Siwe naye muṭateta
Ni kiwingu kiṭapita
Hakiwezi kusaliya.

185. Ṭwalaka siiteleze
Aiṭakapo mpuze
Wala siitenrekeze
Lake kumṭimiziya.

186. Ṭwalaka Mungu meweka
K̇a dharura kutumika
Iwapo mumedhikika
Mumekosa zoṭʰe ṇḍiya.

187. Kushaliki mushinrwapo
Ṭwalaka huwa ni hapo
Na muḍa uiṭowapo
Usiiziḍishe moya.

188. Ṭimiza na masharuṭi
Ya hali piya wakaṭi
Na hukumu ziṭafiṭi
Kabula ya kutumiya.

189. Kuna watʰu huwaṭana
Kisa mara huwawona
K̇a haramu waṭakana
Zipengee huzengeya.

190. Huzengeya muhalili
Fikiriya yambo hili
La k̇azima fahali
Mke k̇enra mpekeya.

191. Na langine kadhalika
Ni k̇a mmoya ṭosheka
Ila kiwa medhikika
Haikupinga shariya.

192. Mke siyowe wa pili
Ni udhiya k̇eli k̇eli
Na ingawa ni halali
Ni uzito kutumiya.

193. Na wanawake si sawa
K̇a wengineyo ni ḍawa
Uṭaiyuṭa kuzawa
Nimek̇ambiya Yahaya.

194. Kuna wanaoridhika
Wangawa wanung'unika
Kuna wangine huwaka
Fununu wakisikiya.

195. Kwongeza si haramu
Walakini ufahamu
Ni kʰuu mno jukumu
Mbali na wake udhiya.

196. Ikiwa sababu iko
K̇a mfano mke wako
Mepowa mikali miko
K̇a dharura za afiya.

197. Labuḍa hana kizazi
La kuzaa haliwezi
Nawe waṭaka pumbazi
Yapo ni ṁana mmoya.

198. Au yale mashughuli
Yeye humpa thaqili
Nawe kusiṭahamili
Huliwezi hilo piya.

199. K̇a dharura ziso buḍi
Usitenre k̇a kasiḍi
K̇engeza wa zaiḍi
Kiṭosheleza mmoya.

200. K̇a mmoya kuṭosheka
Nriyo bora bila shaka
K̇engeza ukiṭaka
Ni kama nilok̇ambiya.

201. Usiwe kiruka mṭo
Khasa kiwa na watoto
Kuna hisabu mzito
Akhera ṭakungojeya.

202. Usiifanya cha nyuki
Hutʰuwi na huḍiriki
Ukishik̇a hushikiki
Mara huwa umeteya.

203. Kiwa umepeṇḍa tunra
Huna buḍi na kupeṇḍa
Mti wake ṭangu kaṇḍa
Wazee waliṫambiya.

204. Nawe kimpeṇḍa mke
Wapeṇḍe wazee wake
Wak̇e mḃako siyepuke
Na hishima kuwekeya.

205. Muhishimu wake mama
Piya babake ḍaima
Kuwadharau si wema
Tono nawe ṭamtiya.

206. K̇a uwovu siwanene
Iṭunge siwatukane
Haṭa kama huyo ṁane
Hishima mewavuṇḍiya.

207. Wewe kaṭu sisubuṭu
Kudharau hao watʰu
Haṭa kama utukutu
K̇ao umeshuhuḍiya.

208. Kiwa ni watʰu matata
Siyo nawo uṭateta
Kheri mbali kuivuta
Na mambo k̇angaliya.

209. Ukiwa una nafasi
La kuwapa sikuwasi
Ila fanya k̇a kiyasi
Siye dewe kakutiya.

210. Kuna wak̇e wa wangine
K̇a kupata waḍengene
Kiwa nawo upembene
Hadhari nakuusiya.

211. Wangine ni watʰu sana
Kaṭu hawakuḍangana
Haṭa kiwa haja una
Haaṇḍami kuk̇ambiya.

212. Hanaṇḍi haṭa nyumbani
K̇a ṁanawe kaṭamani
Kucha watʰu wasidhani
Amek̇enra kutawiya.

213. Ṇḍiyani mukikutana
Huwa na haraka sana
Hamakiniki kunena
K̇a lilo kulikimbiya.

214. Wakiwa wak̇e wa wako
K̇ao hizi sifa ziko
Basi ni bahaṭi yako
Ni hapo pa kuziwiya.

215. Ama wak̇eo wakiwa
Ni wa kupeṇḍa kupowa
Kuwapa hukuzuwiwa
Mkono kuwanyosheya.

216. Usiweke kama aḍa
Kisa ṭak̇eteya shiḍa
Ila wawe si la buḍa
Ni watʰu wahiṭajiya.

217. Wakiwa ni wahiṭaji
Siwangoje kuṭaraji
Wakiwa k̇ako hawaji
Ni sawa kuwapekeya.

218. Ukiwa umewaona
Si watʰu wenye maana
Ni wale wa kuḍangana
Wa kupeṇḍa kupʰapiya.

219. Ziwiya siṭowe chako
Na ṁambiye mke wako
Ila huṭofu sumbuko
Birika mbovu kutiya.

220. Ama wasiyo wazazi
Wajomba na mashangazi
Hapo kuna ngumu kazi
K̇a yetu hini ḍuniya.

221. K̇aṇḍa usiwaṭapiye
Kʰeṭi mbali wangaliye
Ukiyaona mamboye
Ṇḍiya hayak̇ekeleya.

222. Usenre sana karibu
Ṭaivutiya ṭaabu
Ni wengi wa kuharibu
Katika nimezotaya.

223. Ama mashemegi zako
Ḍaḍa zake mke wako
Ṁanangu sivuṇḍe miko
Ilowek̇a na shariya.

224. Usiyonrowe mipaka
K̇a mzaha na dhihaka
Mara mambo hugeuka
Kizaazaa kikaya.

225. Kheri wambiwe muwovu
Kuliko kupata kʰovu
Kheri wambe una wivu
Kuliko kukuvuṇḍiya.

226. Wivu ni kama kiyungo
Ukiziḍi ni ṭewengo
Piya kuyifanya ṭʰongo
Uḍuyuthini hungiya.

227. Na kuukosa kabisa
Ingawa nriyo kisasa
Hiyo si njema siyasa
Ya nyumbani kutumiya.

228. Ni lazima kuwa nawo
K̇a aliyo ni mkeyo
Kikuzumbuwa hunawo
Maṭoni huṭomngiya.

229. Kuwa nawo wa kaḍiri
Hiyo nriyo ḍasiṭuri
Na k̇a mke ni fakhari
K̇a weṇḍe ṭayivuniya.

230. Na fununu ukipata
Kuwa mke ni matata
Siinuke na kuteta
K̇aṇḍa ziḍi k̇angaliya.

231. Simṭukuliye dhana
K̇a kuwa waja hunena
Hilo ni khaṭari sana
Mayuṭoni ṭakutiya.

232. Iziwiye usubiri
Uhakikishe khabari
Ṭena ufanye k̇a siri
Pasi na kupija mbiya.

233. Ikiwa umeṭosheka
Hilo ni yambo hakika
K̇a ṭaraṭibu epuka
Bila sababu kutaya.

234. Sitaye yako sababu
Uṭaziḍi kuharibu
Zitatangaa aibu
Na si wema k̇eneya.

235. Na hilo kisa kutenra
Huna buḍi kuyipinra
Haṭa kama una nyoṇḍa
Siwe nyuma ṭarejeya.

236. Ipinre ipinre mno
Sibaḍili lako neno
Ṁiso ṭapata usono
Yaṭaṭoka mazoweya.

237. Uṭasukikasukika
Kiwa moyo wamṭaka
Fahamu ṭafedheheka
Kiwa huṭoyiziwiya.

238. Iziwiye ikukuse
Mpaka mahaba yese
Penyenye usiyapise
Moyoni kakuruḍiya.

239. Ṁisowe yaṭaonroka
Na wewe uṭaafika
Kuliko kufedheheka
Na izarani kungiya.

240. Lakini nakukumbusha
Kiswa cha Nana Aisha
Vurumai walizusha
Mawi wakamzuliya.

241. Waliyonena ni wengi
Wakafanya na magengi
Na zikao za mitingi
Maḍina zikayeneya.

242. K̇a yambo liso asili
K̇a mke wake Rasuli
Kaṭu halikuwa k̇eli
Ni uvumi walitiya.

243. Ṁangaliye na Mtumi
Alikuwa haaṭami
Aliziwiya ulimi
Mpaka wahayi kuya.

244. Yaṭaka mno hadhari
Katika hizo khabari
Siwe mpesi kukiri
Yambo ukilisikiya.

245. Ṭafiṭi ṭʰafiṭi sana
Haṭa shaka uwe huna
Nripo hapo lako nena
Bila sababu kutaya.

246. Hapa sasa niṭakoma
Wala yoṭʰe sikusema
Lakini ukiyaṇḍama
Haya ṭakusaiḍiya.

247. Niya na yangu dhamiri
K̇aṇḍika k̇a mashairi
Ni k̇eneza khabari
K̇a wenye kuyasikiya.

248. Ni sahali kusikiza
Kaseti moya huweza
Wengi wakapulikiza
Wakasikiza pamoya.

249. Lau kama ni kiṭabu
Wasomaji ni hububu
Wengi huona ṭaabu
Kusikiza mezoweya.

250. Kauli yangu ṭamaṭi
Ni zenu hizi baiṭi
Wavulana mabanaṭi
Nyoṭʰe nawakusuḍiya.

Ṁisho wa uṭeṇḍi. Mtunzi Usṭadh Mahmouḍ Ahmaḍ Abḍulqaḍir (MAU) Lamu-Kenya ṁaka 2004. Umeleṫa Zanzinet na Saleh Barkey ṭarehe February 2005.

Umesawiḍiwa k̇a haṭi hizi kulingana na kiSwahili Asiliya na Mohameḍ Karama, University of Kabianga, Kericho; Usṭadh Mahmouḍ Ahmaḍ Abḍulqaḍir (MAU); na Mbarak Abdulkaḍir wa Lamu, Kenya, leo 05/06/2023.

**Ṭanbihi**: Haṭi hizi zimo k̇enye majaribiyo baḍo zahiṭaji marakibisho kukiyaṇḍika kiSwahili kiṭamk̇avo.

**Maana ya maneno ya kiAmu k̇a kiSwahili Sanifu**

| kiAmu | | Maana kiSanifu | kiAmu | | Maana kiSanifu |
|---|---|---|---|---|---|
| ubeti | | | ubeti | | |
| 15 | Hakumbiriya | Hakutupa | 92 | Kaṭiṭi | Kidogo |
| 18 | Ina | Jina | | Bubwi | Bubu |
| 21 | Jongo | Ya makosa | | Ḍuko | Kiziwi |
| 22 | Sheshegi | Vishindo | 94 | Ṭamuukiya | Utamrukia/kemea |
| | Gogi | Kuvuka mpaka kufikia kudharau | 105 | Una ṁako | Ana hamu |
| 27 | Tutu | Mahindi/ngano | 118 | Makawaṇḍa | Uwanja |
| | Ufu | Nazi | 120 | Mezolinena | Alilolisema |
| 28 | Wangakazaniya | Hata wakishikilia | 125 | Kuṭoṭapasa | Kutosema |
| 29 | Kuṭoeleya | Kutoelewa | 126 | Sini | Chombo cha China |
| 39 | Usimliche | Usimuache | 130 | Aso tʰaa ana ṭʰomomo | Aso hili ana lile |
| | Mche | Muogope | 132 | Sangaliye | Usitizame |
| 43 | Maḍaka | Baraza nje ya nyumba | 135 | Kujeresha | Kutia haya |
| | Kuṭoṭungiya | Kutochungulia | 139 | Kishogo | Kisogo |
| 46 | Toto | Ndogo | 146 | Mewaganya | Yamewaelemea |
| 54 | Weṇḍe | Wenzake | 149 | Igegese | Jilete polepole |
| 72 | Ṭaqiṭiri | Ugumu, ubakhili | | Nyangwani | Jangwani |
| 73 | Ipambe | Jipambe | 158 | Mṭaro | Sababu ya kutafuta ugomvi |
| 75 | Iweke | Jiweke | 175 | Umehiṭi | Umekosa |
| 81 | Huṭuṇḍa | Huchunza | | Kiḍarika | Ikigusika |
| 180 | Tʰotʰotʰo | Matope | | Ṭʰeṭe | Cheche |
| 188 | Kushaliki | Kusairi/kukarabati | 203 | Umeteya | Umeteleza |
| 210 | Dewe | Khasara | 211 | waḍengene | Wamedangana |
| 213 | Hanaṇḍi | Hana njiya | 227 | Ṭewengo | Matatizo |
| 233 | Kupija mbiya | Kupiga mbiyu/ kutangaza | 239 | Penyenye usiyapisa | Upenyo usitoe |
| 237 | Usono | Kupumzika | | | |